# URAIA WA MKRISTO
# (CHRISTIAN CITIZENSHIP-OM-5)

**SULEMANI S. MANGE (MG 1987)**

**NISHANI YA URAIA WA MKRISTO**
**(Christian Citizenship – OM – 5)**

## UTANGULIZI:

Kuna umuhimu gani kwetu wakristo kujifunza nishani ya Uraia wa Mkristo? Tutajifunza nishani ya uraia wa mkristo ili:-

(i) Tujue tunavyotakiwa kuishi chini ya Serikali yetu

(ii) Kuzuia migongano isiyo ya lazima kati yetu na Serikali.

(iii) Tunapokuwa raia wema, watu watamtukuza Mungu na hayo yatakuwa mahubiri ya matendo kama alivyohubiri Danieli huko Babeli. Ni ajabu kwa mkristo kuwa mhalifu, kwani Mungu anamtaka kila mmoja kuwa na tabia takatifu isiyo na mawaa.

Yafuatayo ni mambo muhimu anayotakiwa kuyaelewa mwanafunzi wa nishani ya Uraia wa Mkristo:-

### 1. Ielezee Bendera ya Taifa, Jimbo, AY, Watafuta Njia na ya Kikristo:-

(i) Bendera ya Taifa la Tanzania ina rangi nne:-
Kijani, Bluu, au Samawawi, Nyeusi na Njano
Rangi ya kijani, inasimamia uoto (miti, mimea) wa ncho yetu Rangu ya Bluu, inasimamia bahari, maziwa na mito ya nchi yetu (Bahari yetu inaitwa Bahari ya Hindi, Maziama yetu ni Victoria, Tanganyika, Nyasa, Rukwa, Eyasi, Manyara, Natron, Kitangira) Rangi Nyeusi, inasimamia rangi ya ngizi ya Watanzania walio wengi. Rangi ya Njano, husimamia madini ya nchi yetu (Madini hayo ni dhahabu, almasi, Tanzanite, chumvi, ulanga n.k.)

(ii) Katika nchi yetu, hatuna bendera za mikoa.

(iii) Bendera aya AY ina rangi nne: Nyeupe, Nyekundu, Bluu na Njano.

(a) Rangi nyeupe inasimamia usafi wa tabia au matendo ambao wanatakiwa wawe nao watu wa Mungu (Ufu. 19:8)

(b) Rangi nyekundu husimamia kafara. Yesu alijitoa kafara kwa ajili yetu (Ufu. 5:9), sisi nasi tunatakiwa kujitoa kama kafara iliyo hai mbele za BWANA (Rum. 12:1).

(c) Rangi ya bluu husimamia utii wa amri au maagizo yote ya Mungu (Hes. 15:37-41)

(d) Rangi ya Njano husimamia ubora wa utendaji wa mambo yetu yote. Tunamtumikia Mungu Mkuu, utendaji wetu lazima uwe bora (Ufu. 3:18).

(e) Kuna duara katikati ya bendera inayoonyesha dunia tunamoishi. Wapo malaika watatu wenye tarumbera kwenye duara hiyo. malaika watatu wanaonyesha utumishi. Sisi ni watumini wa Mungu. Tunatakiwa kuupeleka ujumbe duniani mwote (Ufu. 14:6-12).

(iv) Bendera ya Watafuta Njia ina rangi nne: Nyeupe, Nyekundu, Bluu na Njano kama rangi za Bendera ya AY. Maana ya rangi hizo ni sawa na maana za rangi za bendera za AY.

(a) Kuna alama ya pembe tatu katikati ya bendera ya Watafuta Njia. Pembe tatu hiyo inaonyesha kuwa kuna Mungu Baba, Mwana na Mungu Roho Mtakatifu. Maana ya pili ya pembe tatu ni kuwa: Elimu inayotolewa kwa vijana wetu lazima iwe na nyanja tatu muhimu, yaani, elimu ya kiroho, ya kiakili na ya kimwili na elimu ya kiroho ndiyo msingi wa aina zote za elimu.

(b) Kuna ngao ndani ya pembe tatu hiyo inayoonyesha ulinzi wa Mungu kwetu (Efe. 6:16).

(c) Ndani ya angao hiyo kina upanga unaosimamia Neno la Mungu ambalo ni upanga wa Roho (Efe. 5:17)

(v) Hatuna bendera ya Kikristo katika Kanisa letu hapa Tanzania.

**2: Eleza namna ya kupandisha bendera ya Taifa pamoja na bendera nyingine mbili kwenye (a) Kambi ya nje au (Camporee) (b) Siku ya programu ya Watafuta Njia (inayofanyika kanisani) (c) Gwaride la nje uwanjani)**

(a) Unapotaka kupandisha bendera ya taifa pamoja na bendera nyingine mbili kwenye kambi ya nje, iweke bebdera ya taifa kwenye mlingoti wa katikati ya milingoti mingine miwili ya bendera hizo mbili. Mlingoti wa bendera ya taifa uwe mrefu kuliko milingoti mingine. Bendera hizo ziwe mbele ya hema litakapotumika kama ofisi ya kambi.

(b) Unapopandisha bendera ya taifa siku ya programu ya Watafuta Njia itakayofanyikia kanisani, ipandishe mbele ya kanisa au jingo mtakalofanyia programu hiyo. Bendera ya taifa iwe katikati ya bendera hizo mbili.

(c) Unapopandisha bendera ya taif kwenye gwaride pamoja na bendera nyingine mbili, ipandishe kwenye mlingoti mbele ya jukwaa atakalokaa mgeni rasmi. Bendera ya taifa iwe katikati ya bendera nyingine mbili.

3.N.B. Ukipandisha bendera ya taifa pamoja na bendera moja, bendera ya taifa iweke kulia mwa bendera hiyo ya pili. Bendera zikiwa tatu, ya taifa ikanaa katikati.

Bendera zikiwa nne, ya taifa inakaa kulia mwa bendera nyingine zote. Bendera zikiwa tano, inakaa katikati.

Bendera ya taifa inapopandishwa, mpandishaji hutembea kwa ukakamavu kuelekea kwenye mlingoti na anapotaka kuipandisha atapiga filimbi ili kuashiria kuwa bendera ya taifa inataka kupandishwa ili watu wanaotembea au waliokaa wasimame wima wakati wa kupandisha na kutelemsha bendera. Kusimama siyo ibada ya sanamu, bali ni kuonyesha heshima.

3: **Onyesha namna ya kukunja bendera ya Taifa lako na kupiga saluti. Eleza ni lini na wakati gani bendera hiyo onapandishwa**.

(a) Bendera ya taifa la Tanzania inakunjwa vizuri na watu wawili. Kila mmoja anashikilia pembe za amarefu ya bendera, Ncha ya mkono wa kulia, inashikamanishwa na ncha ya mkono wa kushoto. Ndipo ncha mbili alizonazo mtu mmoja anazishikamanisha na ncha mbili alizonazo mtu wa pili. Wanaendelea kukunja namna hiyo hadi hapo itakapokuwa imekunjika kabisa.

(b) Baada ya kuipandisha bendera ya taifa, mpandishaji atarudi nyuma, kinyumenyume, hatua moja na piga saluti, ndipo atageuka nyuma na kuondoka akitembea kwa ukakamavu.

(c) Bendera ya taifa hupandishwa kila siku mbele ya majengo ya Serikali, saa 12.00 asubuhi na kutelemsha saa 12.00 jioni. Bendera ya taifa hupandishwa mbele ya jukwaa uwanjani kama mgeni wa kitaifa atakuja kufanya mkutano hapo.

Kuna bendera ndogo zinazowekwa kwenye magari ya viongozi wa Serikali kama ndani ya gari hilo yumo kiongozi wa Serikali, mwenye wadhifa unaopaswa kupeperusha bendera kweneye gari alimo.

4. **<u>Eleza maana na sababu za wimbo wa taifa na kariri maneno yake.</u>**

Wimbo wa Taifa la Tanzani ni sala ya Taifa kwa Mungu kwa ajili ya Tanzania na Afrika kwa ujumla. Wimbo wa Taifa la Tanzania ni kitambulisho cha Taifa (National Identity), kama ilivyo bendera ya Taifa.

**Wimbo wa Taifa la Tanzania unamaneno yafuatayo:-**

1. Mungu ibariki Afrika, wabariki viongozi wake, hekima umoja na amani, hizo ni ngao zetu, Afrika na watu wake.
   Ibariki Afrika, Ibariki Afrika,
   Tubariki, watoto wa Afrika

2. Mungu ibariki Tanzania, dunisha uhuru na umoja, wake kwa waume na watoto, Mungu ibariki, Tanzania na watu wake.

Ibariki Tanzania, Ibariki Tanzania
Tubariki, watoto wa Tanzania.

5. **<u>Eleza haki na wajibu wa raia wan chi yako:</u>**

(a) Raia wa nchi ya Tanzania ana haki zifuatazo:-

(i) Kuheshimiwa (ii) Kwenda anakotaka (iii) Kufanya anachotaka
(iv) Kukutana mtu yeyote anayetaka (v) Kuabudu dini yoyote anayotaka, mradi havunji sheria.

(b) Wajibu wa raia wa Tanzania ni kuilinda nchi yake.

6. **Ongea na katibu Mtendaji wa Kata, Mkuu wa Mkoa au Kiongozi wan chi yako umwombe akueleze kazi zake.**

Kazi za Katibu Mtendaji wa Kata (ambazo zinafanana na kazi za Mkuu wa Mkoa na wa nchi) ni:-

(i) Kusimamia ulinzi na amani ya eneo analoliongoza akitumia vyombo vya dola.

(ii) Kupanga na kusimamia shughuli za amaendeleo ya eneo analoliongoza akitumia idara za serikali zilizo kwenye eneo lake.

(iii) Kusimamia ukusanyaji wa kodi, mapato naushuru wa aina zote akitumia vyombo vya ukusanyaji kodi, mapato na ushuru wa Serikali.

7. **<u>Andika habari, (Ukurasa mmoja) juu ya mtu mashuhuri katika nchi yako. Taja alivyofanya ili kupata umashuhuri wake.</u>**

Mtu mashuhuri (kwa mawazo yangu mwandishi wa somo hili) niliyemchagua ni Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Yafuatayo ni mambo aliyoyafanya ana kupata umashuhuri alio nao:

(i) Mwalimu Nyerere alianzisha Chama cha TANU kilichodai uhuru wa Tanganyika kwa kipindi kifupi (yaani miaka sita tu ukilinganisha na nchi nyingine zilizochukua miaka zaidi ya 10 hadi kupata uhuru). Zaidi ya hayo, uhuru ulipatikana bila kumwaga damu.
(ii) Baada ya uhuru, Mwalimu Nyerere aliwaunganisha wananchi wa Tanganyika wakawa kitu kiomoja. Hakuna ubaguzi wa kikabila japo kuna makabila 120 katika nchi hii.

(iii) Mwalimu amewafanya Watanzania wajithamini, wanajitambua kuwa wao ni sawa na watu wengine (self realization and self esteem)

(iv) Mwalimu amedumisha amani nchini. Walinzi wa marais wa Tanzania hawatembei na bunduki mikononi kama ilivyo kwa marais wa nchi nyingine. Na marais wa Tanzania wanapostaafu wanaendelea kuishi nchini kwa amani.

(v) Mwalimu amesaidia kupatikana kwa uhuru wan chi nyingine sana hapa Afrika, mfano, Msumbiji, Angola, Zimbabwe, Afrika Kusini, Namibia, visiwa vya Comoro.

(vi) Alisaidia kuleta mwungano wa Tanganyika na zanzibara.

(vii) Alisaidia kuleta nafasi ya kupata elimu kwa kila anayetaka kusona na wale ambao hawakupata nafasi ya kusoma wakati wa ujana wao, waliwapatia nafasi ya kusoma, wakiwa watu wazima.

(viii) Alizaidia kutupatia uhuru wa kuabudu.

(ix) Alisaidia kuanzisha umoja wa ncho za Afrika ya Mashariki, ingawaje ulivunjika baada ya rais Obote wa Uganda kupinduliwa na Idi Amin.

(x) Alisaidia kupatanisha vikundi vya Burundi vilivyokuwa vikipigana.

8. **Fanya mojawapo ya yafuatayo:-**

(a) Orodhesha dondoo kumi, za viongozi wan chi yako zinazoeleweka sana.

(b) Orodhesha sehemu kumi mashuhuri za kihistoria za nchi yako

(c) Orodhesha matukio kumi muhimu ya kihistiria ya nchi yako

9(a) **Dondoo za viongozi wa Tanzania nilizozichagua ni hizi:-**

i) “Ili tuendelee tunahitaji vitu vine, ardhi, Watu, siasa safi na viongozi bora” (Mwalimu Nyerere, Mwongozo wa TANU 1971 – 1972).

ii) “Ulinzi na usalama wa Mtanzania ni wa kila mwananchi na hasa mzalendo” (Mwalimu Nyerere Mwongozo wa TANU 1971 – 1972).

iii) “Ujifunze kusoma wakati ni huu” (Mwalimu Nyerere)

iv) “Maadui watatu wakubwa wa maendeleo yetu ni ujinga, maradhi na umaskini” (Mwalimu NYerere).

v) :Uhuru wa Tanzania hauwezi kuwa kamili hadi hapo afrika yote itakapokuwa huru” (Mwalimu Nyerere)

vi) “Maendeleo ya nchi hayaletwi na fedha, yanaletwa na watu, fedha ni matokeo, wala si msingi wa maendeleo” (Mwalimu Nyerere).

vii) “Elimu ni ufunguo wa maisha” (Mwalimu Nyerere)

viii) “Sera ya uwazi na ukweli” (Rais Mpaka)

ix) “Elimu inayotolewa Tanzania haina budi kuwiana na mazingira yetu” (Mwalimu Nyerere)

x) :Kilio cha kufa na kupona. “Mzee Kawawa.

**<u>ZINGATIA:</u>** (i) Zipo dondoo, mashuhuri katika Biblia, mojawapo ni hizi (i) :Kwa maana jinsi hii, Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwanawe wa pekee, ili kila amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele” (Yohana 3:16). Dondoo hiyo ilisemwa na Yesu.

(ii) “Mlipeni Kaisari yaliyo ya Kaisari na Mungu yaliyo ya Mungu” (Mt. 22:21). Dondoo hii ilisemwa na Yesu.

Zipo dondoo nyingine ndani ya Biblia zinapoeleweka sana. Kitu tunachojifunza kwenye dondoo hizi ni kuwa maneno yetu lazima yawe yale yaliyo na maana ili yakumbukwe na watu kwa urahisi na yawasaidie katika maisha yao. Tusipoteze muda kwa kusema maneno yasiyo na maana bali yale yenye mantiki. Yesu anayapima maneno yetu yote, na kuyaleta hukumuni (Mhu. 12:14).

b) **<u>Orodha ya sehemu kumi maarufu za kihistoria hapa Tanzania ni:</u>**

| | | | |
|---|---|---|---|
| i) | Kondoa Irangi | - | Kuna michoro kwenye mawe mapangoni iliyochorwa, kwa ustadi wa watu wa zamani. Yapo masalio pia ya vifaa vilivyotumiwa na watu hao. |
| ii) | Oldvai George | - | Fuvu la kichwa cha mtu aliyeishi zamani sana liliokotwa hapo. |
| iii) | Lugalo Iringa | - | Kuna ngome ya mfalme Mkwawa aliyepigana na Wajerumani kupinga kuingia kwa Wakoloni. |
| iv) | Kalenga Iringa | - | Kuna kumbukumbu za zana za Wahehe. |
| v) | Ilundamatwe Iringa | - | Kuna mnara mahali walipozikwa maaskari wa Kihehe waliopigana na Wajerumani. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| vi) | Inguruka Arusha | - | Kuna mabaki ya zana za chuma zilizotumiwa na watu wa zamani. Zana hizo zilitengenezwa kwa kutumia teknolojia ya Kitanzania. |
| vii) | Halwego (Handebenzyo | - | Ukerewe – Kuna michoro ya watu wa zamani. |
| viii) | Mapango ya Amboni Tanga | - | Kuna mapango yaliyotumiwa na watu wa zamani. |
| ix) | Dar-Es-salaam | - | Chama cha TANU kilizaliwa hapa 7.7.1954. |
| x) | Bujora Mwanza | - | Kuna makumbusho ya mila za zamani za makabila akadhaa ya Tanzania. |
| xi) | Mlima Kilimanjaro | - | Tarehe 9-12-1961, mwenge wa uhuru uliwekwa juu yam lima Kilimanjaro, kama ishara ya kuleta matumaini kwa mataifa yote ya Africa kuwa kila nchi inatakiwa kujitawala. |

**ZINGATIA:**

(Sehemu maarufu duniani upande wa kiroho ni Bethelehemu, mahali alipozaliwa Yesu, Nazareth, sehemu alipolelewa Yesu, Yordani, mahali alipobatizwa Yesu Golgotha, mahali alipojitoa kafara Yesu, Kafara ambayo imetukumboa.

C: **Mtatukio ya kihistoria ya Tanzania ni:**

i) Kuzaliwa kwa chama cha TANU kilicholeta uhuru TANU ilizaliwa 7/7/1954.

ii) Uhuru wa Tanganyika uliopatikana 9/12/1961

iii) Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ulipfanyika tarehe 26/4/1964

iv) Kuanzishwa kwa Jumuiya ya Africa Mashariki mwaka 1967

v) Kuzaliwa kwa CCM toka vyama vya TANU na ASSP (CCM ilizaliwa tarehe 6/2/1977)

vi) Vitqa vya majimaji, vilivyoongozwa na Kinjikitile dhidhi ya uvamizi wa Kijerumani, mwaka 1905 – 1907. vita hivyo vilitokea Songea.

vii) Maasi ya maaskari wa KAR, ya mwaka 1964, yaliyopelekea kuvunjwa kwa jeshi hilo na kuundwa kwa jeshi la wananchi wa Tanzanaia (JWTZ)

viii) Vita vya Kagera vilivyotokea mwaka 1978 hadi 1979.

ix) Kutangazwa kwa azimio la Arusha tarehe 5/2/1967 lililoleta siasa ya Ujamaa na Kujitegemea.

xi) Watanzania kuhamia kwenye vijiji vya ujamaa mwaka 1974.

xii) Kuzama kwa meli ya MV Bukoba tarehe 21/5/1996

xiii) Kifo cha Baba wa Taifa tarehe 14-10-1999

xiv) Kuanguka kwa train ya abiria tarehe 24-6-2002 kati ya Isagali na Igunga dodoma na kuu watu 283.

**9. <u>Eleza unavyoweza kufanya kama raia wa Tanzania ili kulisaidia kanisa lako na nchi yako.</u>**

Kila mmoja anatakiwa aeleze yale anayofikiria kuwa anaweza kuyafanya ili kulisaidia kanisa na nchi yake. Hii ni kazi ya nyumbani ambayo itasahihishwa.

Utagundua kuwa watu wengi hawana mipango yoyote kwa ajili ya kulisaidia kanisa na nchi yao na hata hawana mipango yao weneyewe. Chanzo cha umaskini kwa watu wengi ni kutokuwa na mipango. Watu wengi wanakabiliana na mambo muhimu katika maisha yao kama dharura. Utakuta mtu hajui ataoa lini na wala hana mipango aliyoipanga ili aoe muda anaotaka. Anapokabiliwa na swala la kuoa analikabili kama dharura, na hali alikuwa anajua kuwa kila binadamu wa kawaida huwa anaoa au kuolewa.

Watu wengi hawapangi mipango ya kazi zao. Utakuta mtu analima mashamba bila kupanga kuwa alime ekari ngapi. Mtu anasema kuwa "nitalima hadi nguvu ziniishe". Kama nguvu zitamuishia baada ya kulima ekari moja hasikitiki na wala hajui kama ekari moja itamtosha maana hana mipango. Washiriki hawana mipango ya kufanya kwa ajili ya kanisa. Wakifanya jambo dogo au wasifanye kabisa hawaumii maana hawana mipango yoyote.

Watu wanaostahili kutokuwa na mipango ni wale waliokufa siyo walio hai. Panga mipango yako binafsi na ya jinsi utakavyofanya kulisaidia kanisa na nchi yako. Mipango siyo nadhiri lakini ni vitu inavyofikiria kuvifanya kwa neema ya BWANA.

10.**<u>Eleza hatua anazozichukua mtu akitaka kupata uraia wa nchi yako</u>**

Zipo aina tatu za uraia zinazotolewa hapa Tanzania, ukitoa uraia wa kuzaliwa na baba na mama watanzania wa kuzaliwa. Aina hizo za uraia ni kama zifuatazo:-

i) **<u>Uraia wa kuandikishwa</u>** (Citizenship by registration)

Uraia huu hutolewa kwa mtu toka nchi za jumuiya ya madola (common Wealth). Mtu huyo atakwenda ofisi ya uhamiaji, naye atapewa fomu zifuatazo ili azijaze.

Fomu A. (b) Fomu ya kiapo cha uaminifu (Oath of Allegience) (c) Fomu ya tamko kuhusu ukaaji (Declaration concerning residence) (d) Fomu ya tamko kuhusu uraia (Declaration concerning Citizenship) Fomu hizo zitapelekwa kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ambaye atatoa hati ya uraia kwa mwombaji akiridhishwa na maombi yake.